JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA

Simu:+255262965679,+255262965676,+255622225618
Barua pepe: ded@kaliuadc.go.tz
Tovuti: www.kaliuadc.go.tz

S. L. P 83
Kaliua Tabora

KDC/M.2/VOL. III/0056/46 14/02/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA WAKUSANYA MAPATO – NAFASI 26.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua anawatangazia Wananchi wote wenye sifa, nafasi ya kazi ya kukusanya mapato kama ifuatavyo:-

1: SIFA ZA MUOMBAJI:-

i). Awe Raia wa Tanzania.
ii). Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.
iii). Awe na Elimu ya kidato cha Nne au zaidi.
iv). Awe na Kitambulisho cha Taifa (**NIDA**) au namba ya Kitambusho cha Taifa (**NIDA**)
v). Awe ni mkazi wa eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.
vi). Awe na mdhamini mwenye kiasi cha fedha au mali isiyo hamishika yenye thamani ya kuanzia TZS 10,000,000/= (milioni kumi) na zaidi. Dhamana ya fedha italazimika kuwasilishwa Halmashauri kupitia akaunti ya amana. Dhamana ya mali isiyo hamishika itathibitishwa kwa kuwasilishwa Halmashauri hati au nyaraka ya umiliki inayotambulika na iliyothibitishwa kisheria kuwa ni mali ya mtoa dhamana.
vii). Awe hajawahi kupatikana na makosa ya jinai au kuhukumiwa kifungo jela katika Mahakama yoyote.
viii). Awe tayari kufanya kazi katika Kata yoyote iliyoko ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.
ix). Mtu yeyote aliyewahi kufanya kazi na halmashauri kisha kuisababishia hasara ya upotevu wa mapato au kudaiwa na halmashauri, **HARUHUSIWI KUOMBA KAZI YA KUKUSANYA MAPATO.**

2: MAJUKUMU YA MKUSANYA MAPATO:-

viii). Kukusanya mapato ya Halmashauri kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato vilivyopo katika eneo la wilaya ya Kaliua kwa kutumia mashine ya kielektroniki (POS).

ix). Kuwasilisha benki kupitia akaunti ya mapato ya halmashauri makusanyo yote yaliyokusanywa ndani ya saa 24 katika siku za kazi au siku ya kwanza ya kazi ya wiki au baada ya sikukuu.

x). Kutoa risiti za mashine ya kielektroniki (POS) kiasi sawa na fedha atakayolipa mlipaji.

xi). Kutunza vifaa vya kukusanyia mapato (POS, rejista) na nyaraka za benki au Halmashauri zinazothibitisha uingizaji wa fedha benki.

xii). Kufanya uhakiki kila siku wa makusanyo ya siku na taarifa ya mashine ya kukusanyia mapato.

xiii). Kuwasilisha Halmashauri mashine ya kukusanyia mapato (POS) kwa ajili ya uchunguzi.

xiv). Kufanya kazi zingine zinazohusu mapato kadri atakavyoelekezwa na Mwajiri.

3: MUDA WA AJIRA

Ajira ya Mkataba ya miezi kumi na mbili kuanzia mwezi Machi 2023 hadi Machi, 2024.

4: MALIPO YA MKUSANYA MAPATO:-

Malipo kwa kazi ya ukusanyaji mapato yatakuwa asilimia 5 (5%) ya makusanyo yaliyokusanywa na kuwasilishwa Benki.

Maombi yatumwe kwa:-
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S. L. P. 83,
KALIUA.

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 27/02/2023 saa 9.30 Alasiri.

W. M. Lindi
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Wilaya

MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA KALIUA S.L.P. 83 KALIUA

Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)